**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG**
**SHULE YA SEKONDARI SUMAYE**

SHULE YA SEKONDARI SUMAYE,
S.L.P. 60,
**KATESH- MANYARA.**
Tarehe………………….

**MAWASILIANO:-**
Simu: **0786083712/0624745412**
**Barua pepe: saulobarhes@gmail.com**

**KUMB. NA. SSS/ADM/JOINING K. I/VOL.VI/2023**
Mzazi/Mlezi wa S.L.P. …………………………….
………………………………………………………….
YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI SUMAYE WILAYA HANANG, MKOA WA MANYARA MWAKA 2023**

Ninafurahi kuwa mwanao ……………………………………………………. amechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika shule hii mwaka **2023,** SUMAYE sekondari ni shule ya kutwa ya mchanganyiko.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **………………..**. Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **……………….** mwisho wakuripoti shuleni itakuwa tarehe………………………..
Ni muhimu mwanao kuripoti tarehe hiyo ili ashiriki kikamilifu katika utaratibu ulioandaliwa na shule. **KARIBU SANA**

Ni matumaini yangu kuwa mwanao atatumia vizuri nafasi hii na kwamba ataweka **JUHUDI** na **MAARIFA** ya hali ya juu ili aweze kufanikiwa katika masomo na shughuli nyingine muhimu kama vile uzalishaji mali, usafi na michezo kwa kipindi chote cha uanafunzi wake hapa shuleni.

Shule hii ipo katika Wilaya ya **HANANG**, Mkoa wa **MANYARA.** Ipo kilomita 25 kutoka mji wa **KATESH**. Shule ipo katika kata ya **GENDABI – KIJIJI CHA SARJANDA**. Kwa wale wanaotoka mikoani usafiri unapatikana katika kituo cha mabasi cha **KATESH**, nauli ni Tsh 2500 hadi shuleni.

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana **SUMAYE** Sekondari.

**…………………….**
**SB, BARABOJICK**
**MKUU WA SHULE**

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.0 SARE ZA SHULE (wasichana)**

1. Blauzi mbili (2) light blue mikono mifupi
2. Sketi 2 (marinda madogo ya kawaida) au suruali kwa waislamu
3. Jozi mbili za viatu vyeusi visivyo na visigino virefu vya kufunga na kamba.
4. Jozi mbili za soksi nyeupe.
5. Sweta ya rangi ya light blue yenye shingo ya "V" isiyopasuliwa mbele
6. T- shirt ya shule, utaratibu utatolewa mara baada ya wanafunzi kuripoti
7. Raba jozi moja na nguo za michezo yaani bukta nyekundu, t-shirt ya bluu

**Wavulana**

1. Suruali 2 za light blue
2. Shati 2 nyeupe za mikono mifupi
3. Jozi mbili za viatu vyeusi vya kufunga na kamba, visiwe buti.
4. Jozi mbili za soksi ya khaki
5. Sweta ya rangi ya light blue yenye shingo ya "V" isiyopasuliwa mbele
6. T- shirt ya shule, utaratibu utatolewa mara baada ya wanafunzi kuripoti
7. Raba jozi moja na nguo za michezo yaani bukta ya kijani, t- shirt ya njano

**NB**: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo ambazo siyo sare ya shule. Ukaguzi utafanyika mwanafunzi anaporipoti shuleni. Kila mzazi/mlezi atawajibika kumshonea mwanaye sare hizi kabla ya kuripoti, Kwa lengo la kurahisisha zoezi hili la sare kipande cha kitambaa kwa ajili ya suruali na sketi kimeambatanishwa na fomu hii.

**3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Technolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Utatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara utakaporipoti shuleni.

**(a) HESHIMA KWA WAKUBWA WANAOKUZIDI UMRI**

(i) Kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita au kuingia mahali ulipo
(ii) Kutumia lugha nzuri wakati wote.
(iii) Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wengine katika kazi.
(iv) Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote
(v) Kuitikia mara moja na kukimbilia aliko mkuu anayekuita.
(vi) Kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha ya Taifa
(vii) Kukaa kimya darasani na kutoka kwa ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko darasani.
(viii) Mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo ndani na nje ya shule.

**(b) BAADHI YA TABIA ZISIZORUHUSIWA KWA MWANAFUNZI**

(i) Kuvuta sigara, kutumia dawa za kulevya, pombe n.k.
(ii) Kufuga kucha ndefu, ndevu au nywele ndefu/chafu
(iii) Kuvaa mavazi yasiyokubalika au yasiyo ya heshima
(iv) Uasherati, wizi, utapeli, udanganyifu, uongo n.k.
(v) Kupiga kelele uwapo darasani au kwenye shughuli za nje ya darasa

**(c) SARE**

Unapaswa kuwa na sare za shule kwa mshono uliokubalika na kwa wakati wote katika mazingira yafuatayo: -

(a) Wakati wa masomo darasani
(b) Safari zote za nje ya shule kwa jina la shule
(c) Unapotoka au kwenda likizo
(d) Sare za michezo kwa siku za michezo shuleni au nje ya shule

4.0 **MIPAKA YA SHULE**

a) Unapaswa kufahamu mipaka ya shule na kutotoka nje ya mipaka hiyo.
b) Kibali maalum ya kutolea ruhusa kitatolewa na mwalimu wa zamu au mwalimu wa malezi na itaidhinishwa na Mkuu wa shule kila unapokwenda nje ya shule.

(i) Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea maeneo yafuatayo bila kuwa na sababu ya msingi au ruhusa: -
(a) Ofisi ya Walimu
(b) Ofisi ya Mkuu wa shule
(c) Nyumba za walimu au wafanyakazi wasio walimu bila ruhusa maalum.

(iv) Hairuhusiwi kabisa kwa wanafunzi kutembelea
(a) Vilabu vya pombe
(b) Majumba ya starehe
(c) Nyumba za kufikia wageni (Guest House)

5.0 **MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

**(i)** WIZI
**(ii)** UASHERATI
**(iii)** ULEVI WA AINA YOYOTE
**(iv)** UVUTAJI SIGARA AU BANGI
**(v)** MAKOSA YA JINAI
**(vi)** KUPIGANA AU KUPIGA
**(vii)** KUHARIBU KWA MAKUSUDI MALI ZA SHULE
**(viii)** KUDHARAU BENDERA YA TAIFA
**(ix)** UTORO
**(x)** KUPATA AU KUSABABISHA MIMBA
**(xi)** KUTOA MIMBA
**(xii)** KUOLEWA
**(xiii)** UTOVU SUGU WA NIDHAMU KWA UJUMLA
**(xiv)** **KUMILIKI SIMU AU LAINI YA SIMU**

## 6.0 USAFI

Usafi ni wajibu wa kila mwanafunzi kama sehemu ya maisha yake ya kila siku, hivyo mwanafunzi atahusika na: -

(a) Usafi binafsi wa mwili na mavazi
(b) Usafi wa maeneo (viwanja vya shule)
(c) Usafi wa madarasa, vyoo, jiko na stoo ya kuhifadhia mazao na vifaa vya shule
(d) Ni marufuku mwanafunzi kutupa taka ovyo au kupita karatasi zikizagaa bila kuziokota

## 7.0 MAHITAJI YA CHAKULA, TAALUMA NA MAZINGIRA

### A. CHAKULA

Shule hii ni ya kutwa na hivyo muda mwingi wanafunzi watakuwa wanakaa katika makazi ya wazazi/walezi wao au hostel, lakini kwa muda watakapokuwa shuleni watahitaji kunywa uji wa asubuhi na chakula cha mchana. Kwa mantiki hiyo wazazi/walezi wameweka michango ya chakula hicho kwa kila mwanafunzi kama ifuatvyo: -

(i) Mahindi debe tatu (3) kwa mwaka kwa wanafunzi wa kutwa
(ii) Maharage debe moja na nusu ($1^1/_2$) kwa mwaka kwa wanafunzi wa kutwa
(iii) Mchango wa chakula Tsh 56,000/- kwa mwaka (fedha hizi zitatumika kununua kuni, mafuta ya kupikia, sukari, chumvi, nyanya, vitunguu na mchele, posho mpishi n.k) kwa wanafunzi wa kutwa
(iv) Gharama ya chakula kwa wanafunzi wanaoishi hostel itakuwa kama ifuatavyo: -
    - Mahindi debe nane (8) kwa mwaka au debe nne (4) kwa muhula
    - Maharage debe tatu (3) kwa mwaka au debe na nusu ($1^1/_2$) kwa muhula
    - Fedha za chakula shilingi 187,900/- kwa mwaka au 93,950 kwa muhula
(v) Vyombo vya chakula kama vile kikombe cha uji, sahani na kijiko.

**Fedha taslim hazipokelewi shuleni, hivyo kila mzazi/mlezi anatakiwa kuweka fedha za chakula katika akaunti ya kamati ya chakula cha wanafunzi SUMAYE sekondari. Vile vile wanafunzi wanaoishi HOSTEL wataweka fedha zao za chakula na mahitaji mengine kwenye akaunti ya HOSTEL SUMAYE SEKONDARI kama ifuatavyo: -**

- ✓ Kwa wanafunzi wote wa kutwa akaunti namba itakayotumika ni: **41010006291 – JINA CHAKULA SUMAYE SEKONDARI**
- ✓ Kwa wanafunzi wa HOSTEL akaunti namba itakayotumika ni: **41010010246 – JINA HOSTEL SUMAYE SEKONDARI**

### B. TAALUMA

Kwa mujibu wa sera ya elimu iliyoanza kutekelezwa toka mwaka 2016, elimu ya sekondari kwa kidato cha kwanza hadi cha nne imefanywa kuwa elimu msingi na hivyo kutolewa bila ya malipo ya ada au michango mengine kama ilivyozoeleka hapo awali, hata hivyo wazazi kama wadau wa elimu nchini wameona ni vema kuendelea kusaidiana na serikali hasa katika maeneo ambayo yameonyesha upungufu. Kwa mantiki hiyo wazazi wa shule ya sekondari ya **SUMAYE** kwa hiari yao wamepitisha mchango wa taaluma wa Tsh 10,000/- kwa mwaka ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa walimu katika baadhi ya masomo kama vile English, chemistry n.k

Vilevile kila mzazi/mlezi anawajibika kumnunulia mwanae vifaa vingine vya taaluma kama ifuatavyo: -

(i) Daftari kubwa tisa (09) countbook quire 2 au 3
(ii) Daftari ndogo za kawaida za kutosha kwa ajili ya mazoezi ya darasani

(iii) Kalamu za kutosha
(iv) Penseli kwa ajili ya michoro
(V) Rimu moja kwa ajili ya majaribio na mitihani ili kuimarisha taaluma na kuepuka kuchana madaftari
(V) Mkebe wa hesabu, ufutio, rula n.k.
(vi) Begi zuri ya kubebea madaftari na vifaa vyake vingine

C**. MAZINGIRA NA SHUGHULI ZA SHAMBA**

Moja ya mambo ambayo tunayazingatia sana hapa shuleni ni pamoja na utunzaji wa mazingira hivyo kila mwanafunzi anapokuwa shuleni atatakiwa kuwa na bustani ya maua na miti ya kutunza, ili kuifanya shughuli hii kikamilifu kila mwanafunzi anatakiwa kuleta vifaa vifuatavyo: **-**

(i) Ndoo safi ya lita kumi (10) kwa ajili ya kuchotea maji
(ii) Jembe lenye mpini imara kwa ajili ya shughuli za shamba na kupalilia maua na miti.
(iii) Fagio moja aina ya chelewa
(iv) Kwanja kwa ajili ya kufyekea majani

8.0 **MATUMIZI NA UTUNZAJI WA MALI YA SHULE NA MAZINGIRA**

a) Kila mwanafunzi anatakiwa kutumia na kutunza vizuri mali za shule kama vile majengo, viti, meza, madawati, majembe, ndoo, vitabu, vifaa vya madarasani n.k.
b) Weka mazingira ya shule katika hali ya usafi na ya kuvutia. Okota karatasi au uchafu wowote, pita kwenye njia za miguu, usikatishe kwenye njia za miguu isiyoruhusiwa, usikatishe ovyo na kukanyaga majani au maua.

9.0 **UTORO**

Mwanafunzi ambaye hatahudhuria shule bila taarifa atahesabiwa ni mtoro. Taarifa kuhusu mwanafunzi asiyehudhuria kutokana na matatizo yoyote lazima iwasilishwe shuleni siku hiyo ya matatizo kwa mwalimu wa darasa, mwalimu wa zamu, mwalimu wa malezi au mkuu wa shule na mzazi au mlezi atakayetambuliwa na shule kulingana na fomu ya usajili. Aidha ijulikane kwa kila mmoja kuwa kwa mujibu wa sheria za shule utoro wa siku 90 mfululizo unafuta usajili wa mwanafunzi shuleni.

**…………………………**
**SB, BARABOJICK**
**MKUU WA SHULE**

**FOMU A**

**HATI YA MAKUBALIANO**

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari SUMAYE,
S.L.P 60,
**KATESH.**

**YAH: KUKUBALI KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE**

Mimi …………………………………………………………………………..

Nakubali nafasi ya kidato cha ………………. niliyopewa katika shule yako. Nayakubali masharti na kuwa nitatii sheria za shule hizo zilizoko na zile zitakazotolewa kwa muda wote wa masomo yangu. Naahidi kuwa nitawaheshimu na kuwatii walimu wote na wafanyakazi kama walezi wangu. Naahidi kuwa nitatii wale wote watakaoteuliwa au kuchaguliwa kuwa viongozi wangu kwa mujibu wa sheria.

Naahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mwaminifu. Vilevile naahidi kuwa nitajielimisha kwa nguvu na akili zangu zote kwa manufaa yangu binafsi na Taifa langu. Natambua kuwa nikikiuka ahadi hizi nitapoteza nafasi yangu hapa shule.

JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………………….
SAHIHI ……………………………………………………………………….
JINA LA MZAZI/MLEZI ……………………………………………………
SAHIHI ……………………………………………………………………….
Anwani ya Mzazi /Mlezi ……………………………………………………...
…………………………………………………………………………………
Simu Na…………………………………………………
Namba ya kuandikishwa ……………….. Tarehe ……………………………….
Darasa ulilopangwa ………….............
Jina la Mwalimu Mlezi ………………………………… Sahihi ……………….. Tarehe ……………………

KWA MATUMIZI YA OFISI
JINA LA MKUU WA SHULE……………………………………………………..
SAINI NA MUHURI …………………………………..
TAREHE …………………………..

**FOMU B**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

SHULE YA SEKONDARI SUMAYE
S.L.P 60
KATESH.
Kumb.Na.SSS/ADM/VOL.VI/2023

**FOMU YA MAPOKEZI SHULENI – MAELEZO KUHUSU MWANAFUNZI**

Sehemu A: Ijazwe na mwanafunzi

(1) Jina la mwanafunzi (majina matatu)…………………………………………………………………………….
(2) Taifa ……………………………………………………………………………..
(3) Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………….. (4) Dini………………………………………………………………………………
(5) Shule ya msingi anayotoka …………………………………………………….
(6) Umbali kutoka nyumbani hadi shuleni (weka katika km)……………………… (7) Ulemavu au udadhaifu wenye uthibitisho kama upo
………………………………………………………………………………………

SEHEMU B: IJAZWE NA MZAZI / MLEZI)

(1) Jina la mzazi /mlezi (majina matatu)
………………………………………………………………………………………
(2) Mahali unapoishi Kata ……………………. Kijiji ……………………………
(3) Anuani ya mzazi/mlezi ………………………….. Namba ya simu ………………………………..
(4) Kazi ya mzazi / mlezi ………………………… Mahali anapofanya kazi na anwani
……………………………………………………………………………

Ndugu wawili wa karibu (badala ya mzazi/mlezi):-

(a) Jina ……………………………………………………………………………
Anwani ………………………………………………………………………………
Simu namba ……………………………………………………………………….
Uhusiano wake na mzazi/mlezi ……………………………………………………..
(b) Jina ……………………………………………………………………………
Anwani ………………………………………………………………………………
Simu namba …………………………… Uhusiano wake na mzazi /mlezi
………………………………………………………………………………………..

Jina la mzazi /mlezi ………………………………………………………………… Tarehe ………………………….. Sahihi …………………………...

**FOMU C**

**Shule ya Sekondari SUMAYE,**
**S.L.P 60,**
**KATESH.**

**AHADI / MKATABA WA MWANAFUNZI**

Mimi mwanafunzi (majina matatu) ……………………………………………………

Ninaahidi kufuata taratibu na sheria zote za shule ikiwa ni pamoja na kutokushiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.

Saini ………………………. Tarehe …………………………

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi mzazi/mlezi wa mwanafunzi

………………………………………………………………………………………

Kidato cha …………………………. mwaka ……………………………………...

Ninakiri kukubaliana na sheria, kanuni, michango ya shule na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. Nimesoma/somewa na kuyaelewa vema na kwamba nitayatekeleza kikamilifu kwa kipindi chote mwanangu atakachokuwa katika shule ya SUMAYE Sekondari.

Jina la mzazi/mlezi …………………………………………. Saini ………………. Tarehe ……………………….

KWA MATUMIZI YA OFISI

JINA LA MKUU WA SHULE……………………………………………………..

SAINI NA MUHURI …………………………………..TAREHE …………………………